



TIST HABARI MOTOMOTO OCTOBER 2025

www.tist.org. Email: info@tist.org Tel. +255784-537720



Photo 1: Nyabihuye cluster meeting

In this newsletter, we are going to have;

- I. Small Group eligibility Requirement
- II. Success story from a TIST Farmer Basil Peter Temu

Small Group eligibility Requirement

Your Small Group should meet the following requirements to qualify for the TIST Program: They are important in our TIST activities and in achieving big results. When the Small Group's information is accurate, and the Small Group is eligible for payment, TIST earns trust and a good reputation in the Carbon Market, which increases the value of TIST carbon. If your Small Group does not complete these requirements, your carbon may not be able to be sold in the Carbon Market, resulting in less Profit Share for all TIST farmers.

Your Small Group should meet the following requirements to qualify for payments.

- There should be 6 to 12 members in your Small Group from at least three different families.
- Each Small Group member must be willing to follow the TIST Values.
- Each Small Group member is required to sign the Greenhouse Gas contract.
- Baseline information must be collected and accurate.
 - Each Small Group member should be able to provide proof of land ownership or control of land where they will plant or have planted TIST trees.
 - Each Small Group member should provide information on whether any activities were displaced or moved on their farms, like buildings or farming activities.
- Each Small Group member should say if their land has been forested anytime since 1990.
- Small Groups must meet the requirements governing operations of regulating bodies (Clean Development Mechanism (CDM) or Verified Carbon Standards (VCS). Some of the rules require Small Groups to keep trees in the grove alive for 60 years or longer.
- Each active grove in the group should have been quantified in the last 18 months.
- Each active grove should have a good boundary of their land taken.
- Groves should not count trees that were planted before the members were involved in TIST as TIST trees.
- Groves should not have any Eucalyptus trees counted for TIST planted after 2022.
- Each Small Group member should review and sign each voucher.
- Each Small Group member signing the voucher should be included in the GHG contract.

II. Success story from a TIST Farmer Basil Peter Temu

Basil Peter Temu a TIST Farmer from Mkoka Cluster of the Makao Mapya Farm Group with TIST number: 2004TZ487. I joined TIST Program in 2000 after being encouraged by TIST representatives who were present in our area by that time.

Among of the important things I was taught from TIST were;

- Leadership that is Rotational after every week in our Small Group and every four months in the Cluster the position you have is replaced by the other group member. (That means the leadership in TIST Group or Cluster is equal to all group members not for some special people).
- Low Budgets, Big Results is one of the TIST Value that helps me a lot in doing my work especially in my small farm where I have planted trees while I use the same farm doing Conservation Farming in which I get more yields.
- Mixing different types of soil for planting seeds following the measurements; At first, I only knew that you dig a hole, put fertilizer, watering then you put the seeds and continue watering the seeds in the pots/bags. Unfortunately, I was wrong with my assumptions; instead what you need is to know the correct measurements of how to mix the soil. I did practice on this after training, mixing fertile soil with sandy soil and manure following the measurements and obtained good results in my nursery.

My Farm is located around my home area it is 3 acres in size and has a number of 188 trees of the following types: Eucalyptus, Neems, Lucinar, michongoma, mango tree, Jacaranda, Accacia, Albizia Christmas tree, Tamarid, melia, Guava, citrus, SSP and umbrella tree.

In the previous rainy season, I planted guava, mango, orange and passion fruit. The benefits I get from my trees include fresh air and shade, firewood, fruit, every year my family have a plan and a budget of adding trees in our farm at least 20 trees or more. Apart from farming, I am also doing other businesses like; raising pigs, cows and chickens (using local methods) with the aim of earning income, food and fertilizer for trees and Conservation Farming. I also get benefits from livestock keeping; For example, the sale of milk, cows and pigs allows me to manage well my family such as paying for the children school needs.

Other benefits I get from TIST includes; regular training through the HMM newsletter and various TIST seminars as well as the assurance of entering the carbon business.

Makao Mapya Farm Group has previously received a pre-payment vouchers from TIST based on the number of trees our quantified. The money we received helped the Group members increase the number of trees in our farms; I started beekeeping, fish ponds, and also the money encouraged other surrounding community members to join TIST and start planting trees.

TIST HABARI MOTO MOTO

TIST has helped me meet different Farmers from all over our country through various trainings that joining Farmers together; this has made us have closer communication

Now I can educate the community around me on the importance of caring for our environment protecting, respecting and developing natural vegetation and planting more



Photo 2: Basil's cow, a TIST Farmer




Photo 3: Basil with his cows

NOTE:

TIST Farmer – you are NOT required to contribute money or anything to a TIST employee during the execution of their duties on your farm. If any TIST employee asks you to pay any amount of money, please contact your TIST country management team member.

TIST HABARI MOTO MOTO

TIST Values

As TIST Family we have our Values which most of TIST Small Groups know and practice. We always reflect on these Values and to ensure that we all are truly living by them. The success of TIST is based on the integrity and effort of individual members within TIST. What we can achieve depends on each of us following these Values;

Who are we?

- (i) We are Honest
- (ii) We are Accurate
- (iii) We are Transparent
- (iv) We are Servants to each other
- (v) We are Mutually Accountable to Each Other and
- (vi) We create Low Budget/ cost, yet we achieve Big Results

How we do things that other people can see

- 1) We are committed
- 2) We do our work in small groups
- 3) We seek and use the best way
- 4) We use our minds and hands.

What do we do?

- 1) We plant different species of trees for long -term
- 2) We find ways to improve our health
- 3) We practice Conservation Farming
- 4) We do other projects and businesses (sustainable agriculture, nurseries, citrus growing, dairy goats and farming, chickens, bee keeping, fishponds and fish keeping, silkworm farming etc.)
- 5) We sell carbon credits

What do we create?

- 1) We create team work - by doing things this way; we end up working as a team.
- 2) We create capacity - we create organization, strength, and a system that is strong.
- 3) We create enjoyment - we see results, we accomplish big things that we enjoy.
- 4) We create Big Results - In Conservation Farming and from other projects and business that we do.
- 5) We create Low Budget/Cost, yet we achieve big results.



TIST HABARI MOTOMOTO OKTOBA 2025

www.tist.org. Email: info@tist.org Tel. +255784-537720



Picha 1: Mkutano wa Klasta Nyabihuye

Katika jarida hili, tutakuwa na:

- (I) Mahitaji ya Kustahiki kuwa Kikundi Kidogo
- (II) Hadithi ya mafanikio kutoka kwa mkulima wa TIST Basil Peter Temu

TIST HABARI MOTO MOTO

I. Mahitaji ya Kustahiki kuwa Kikundi Kidogo

Kikundi chako Kidogo kinapaswa kukidhi mahitaji yafuatayo ili kufuzu vigezo kwenye Mpango wa TIST: Jambo hili ni muhimu katika shughuli zetu za TIST na katika kufikia matokeo makubwa. Kikundi Kidogo kikiwa na taarifa sahihi, na kikitimiza vigezo vya kustahiki malipo, TIST inaaminiwa na inapata sifa nzuri katika Soko la Kaboni, jambo ambalo huongeza thamani kwenye kaboni ya TIST. Ikiwa Kikundi chako Kidogo hakitakamilisha mahitaji haya, kaboni yako haitaweza kuuzwa katika Soko la Kaboni, na hivyo kusababisha Mgao wa Faida kuwa kidogo kwa wakulima wote wa TIST.

Kikundi chako Kidogo kinapaswa kukidhi mahitaji yafuatayo ili kupata malipo.

- Kikundi chako Kidogo kinapaswa kuwa na wanachama 6 hadi 12 kutoka angalau familia tatu tofauti.

- Kila mwanakikundi Kidogo lazima awe tayari kufuata Maadili ya TIST.

- Kila mwanachama wa Kikundi Kidogo anatakiwa kutia saini mkataba wa Greenhouse Gas.

- Taarifa za awali lazima zikusanywe kwa usahihi.

- o Kila mwanachama wa Kikundi Kidogo anapaswa kuwa na uwezo wa kutoa uthibitisho wa uniliki wa ardhi ambapo watapanda au wamepanda miti ya TIST.

- o Kila Mwanakikundi Kidogo anapaswa kutoa taarifa kama kuna shughuli zozote zilihamishwa au kuondolewa kwenye mashamba yao, kama vile majengo au shughuli za kilimo nk.

Kila mwanachama wa Kikundi Kidogo anapaswa kusema kama ardhi yao imekuwa na misitu miaka 10 iliyopita.

- Vikundi Vidogo lazima vitimize mahitaji ya uendeshaaji wa mashirika ya udhibiti (Mfumo safi wa Maendeleo (CDM) au Viwango vya Udhibiti wa Kaboni (VCS) Baadhi ya sheria zinataka Vikundi Vidogo kutunza miti shambani iwe hai kwa miaka 60 au zaidi.

- Kila shamba hai katika kikundi linapaswa kuwa limehesabiwa ndani ya muda wa miezi 18 iliyopita.

- Kila shamba linapaswa liwe limechukuliwa mpaka wake vizuri.

- Miti iliyopandwa kabla ya washiriki kujiunga na TIST haipaswi kuhesabu kama miti ya TIST.

- TIST haitahesabu miti ya Mikaratusi iliyopandwa baada ya mwaka 2012

- Kila mwanachama wa Kikundi Kidogo anapaswa kukagua na kutia sahihi kila vocha.

- Kila mwanachama wa Kikundi Kidogo anayetia saini vocha lazima aorodheshwe kwenye mkataba wa GHG.

II. Hadithi ya mafanikio kutoka kwa mkulima wa TIST Basil Peter Temu;

Basil Peter Temu wa Klasta ya Mkoka - Kikundi cha Makao Mapya Farm chenye namba ya TIST: 2004TZ487. Nilijiunga na mradi wa TIST mwaka 2000 baada ya kuhamasishwa na wawakilishi wa TIST waliokuwepo kwenye maeneo yetu.

Miongoni mwa mambo muhimu niliyofundishwa (nikiwa siyajui kabisa) ni juu ya;

Uongozi ambao ni wa mzunguko kila wiki unapisha nafasi uliyo nayo na mwanachama mwingine anachukua hiyo nafasi kwenye Kikundi; pia kila baada ya miezi minne kwenye Klasta (kwamba ukiwa TIST uongozi wa Kikundi au Klasta ni wa kupokezana, sio wa mtu mmoja maalum).

Bajeti ndogo, Matokeo Makubwa ndio falsafa ambayo inanisaia sana katika kumiliki shamba langu dogo la miti.

Uchanganyaji wa aina za udongo wa kupandia mbegu na viwango vyake. Awali nilijua tu kwamba unachimba shimo, kuweka mbolea na maji kisha kuweka mbegu na kuendelea kuimwagilia mbegu kwenye viriba. Kumbé unahitaji kufahamu vipimo sahihi vya namna ya kuchanganya udongo. Nimefanya kwa vitendo kuchanganya udongo kwa vipimo na nimepata matokeo mazuri.

Shamba langu la miti lililopo eneo la nyumbani lina ukubwa wa ekari 3 lina idadi ya miti 188 aina ya; mikaratusi, miarobaini, luciner, michongoma, miembe, mijakalanda, mijohoro, mikenge maji, mikirimasi, mikungugu, mikwaju, mimelea, mipapala, mipera, misorosofi, mistafeli, michungwa, SSP na miashoki.

Miti niliyoipanda kwa msimu wa mvua uliopita ni ya matunda aina ya mipera, miembe, michungwa na mistafeli.

Faida kubwa ninayoipata kwenye miti yangu ni pamoja na hewa na vivuli safi, kuni, matunda vocha kutoka mradi wa TIST, mafunzo ya mara kwa mara kupitia gazeti/jarida la HMM na semina mbalimbali za TIST pamoja na uhakika wa kuingia kwenye biashara ya hewa ya kaboni.

Mpango wa kuendeleza mradi wa miti ni endelevu katika familia yangu ambapo kila mwaka tunaendeleza zoezi la upandaji miti angalau kila mwaka miti 20 au zaidi.

Mbali na kilimo pia nina miradi mingine ninafanya nayo ni ufugaji wa nguruwe, ng`ombe na kuku wa kienyeji (kwa njia za kienyeji) kwa lengo la kujipatia kipato, lishe na mbolea kwa ajili ya miti na Kilimo Hai.

Makao Mapya Farm Group ilishawahi kupata vocha kwa ajili ya malipo ya awali kutoka mradi wa TIST kutokana na idadi ya miti iliyohakikiwa. Malipo tuliyoipata yalisaidia wanaKikundi kuboresha zoezi la upandaji miti, kufuga nyuki, bwawa la samaki, na kusaidia kuhamasisha jamii inayotuzunguka kupanda miti.

Chanzo kikubwa cha biashara niliyo nayo ni sehemu ya matokeo ya elimu niliyopata kutoka TIST. Kwa mfano mauzo ya maziwa, ng`ombe, mazao na nguruwe zinaniwezesha kuongeza bidhaa dukani na kulipia mahitaji ya watoto shuleni.

TIST HABARI MOTO MOTO

Kilimo hai kilionekana kwangu kama njia pekee ya kutokutumia eneo kubwa kwa mazao machache bali ninatumia eneo dogo kwa matokeo makubwa ya uzalishaji yanayonipa nafasi ya kupanda miti. Elimu hii nimeipata kutoka TIST kupitia kwa mfanyakazi wa klasta.

Kwa ujumla tangu nimejiunga na mradi wa TIST nimepata mafanikio makubwa kama nilivyoeleza hapo juu pamoja na;


Kulinda, kuheshimu na kuendeleza uoto wa asili na wa kupanda miti kutokana na manufaa makubwa ninayoyapata.

TIST imenisaidia kukutana wakulima mbalimbali kutoka pande zote za nchi yetu, hii imetufanya kuwa na mawasiliano ya karibu zaidi

Sasa ninaweza kuelimisha jamii inayonizunguka juu ya maana wa utunzaji wa mazingira yetu.



Picha 2: Ng'ombe wa Mkulima wa TIST Basil



Picha 3: Mkulima wa TIST Basil akiwa na Ng'ombe wake

KUMBUKA:

Mkulima HUTAKIWI kuchangia fedha yoyote au kitu chochote kwa mtumishi wa Mradi wakati wa utekelezaji wa majukumu yake shambani kwako. Endapo mtumishi yoyote atakuomba kitu chochote au fedha kiasi chochote, jiridhishe kwanza kwa kuwasiliana na uongozi wa Mradi wa TIST kabla ya kutekeleza ombi hilo.

TIST HABARI MOTO MOTO

MAADILI YA TIST

Kama Familia ya TIST tuna Maadili yetu ambayo wengi wa Wanavikundi Vidogo vya TIST wanayajua na kuyatekeleza. Daima tunatafakari juu ya Maadili haya na kuhakikisha kwamba sote tunaishi kulingana nayo. Mafanikio ya TIST yanatokana na uadilifu na juhudi za wanachama binafsi ndani ya TIST. Tunachoweza kufikia inategemea kila mmoja wetu kufuata Maadili haya;

Sisi ni Nani?

- 1) Sisi ni waaminifu.
- 2) Sisi tunatoa taarifa sahihi.
- 3) Sisi ni wawazi
- 4) Sisi tunatumikiana.
- 5) Sisi ni wawajibikaji
- 6) Bajeti Ndogo, Matokeo Makubwa

Jinsi tunavyofanya mambo ambayo watu wengine wanaweza kuona

- 1) Sisi tunajitolea.
- 2) Tunafanya kazi zetu katika vikundi vidogovidogo
- 3) Tunatafuta na kutumia njia bora
- 4) Tunatumia akili na mikono yetu.

Tunachofanya

- 1) Tunapanda aina mbalimbali za miti itakayodumu kwa muda mrefu.
- 2) Tunafanya mambo kuboresha afya zetu.
- 3) Tunafanya Kilimo Hai.
- 4) Tunafanya miradi na biashara zingine.
- 5) Tunafanya biashara ya hewa ya kaboni.

Tunafanya.

- 1) Tunaunda kazi ya timu—kwa kufanya mambo kwa njia hii; tunaishia kufanya kazi kama timu.
- 2) Tunajenga Uwezo-tunaunda shirika, nguvu, na mfumo ambao ni imara.
- 3) Tunafanya mambo yanayotufurahisha-tunaona matokeo, tunatimiza mambo makubwa ambayo tunafurahia
- 4) Tunafanya mambo yanayoleta matokeo makubwa-matokeo makubwa ya upandaji miti. matokeo makubwa katika Kilimo Hai na matokeo makubwa kutokana na miradi na biashara zingine tunazofanya.
- 5) Tunatumia gharama ndogo za Utawala, lakini tunapata matokeo makubwa.